**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO**

Kumb. Na. AB.259/265/01/33 02/02/2026

## TANGAZO LA KAZI YA UKUSANYAJI WA MAPATO NAFASI 26.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauriya Wilaya ya Nsimbo kwa mamlaka aliyonayo kupitia kifungu cha 31 na 33 cha sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa anawatangazia Watanzania wote wenye sifa kutuma maombi ya kazi ya kukusanya mapato ya Halmashauri.

**NAFASI YA KAZI ; MKUSANYA MAPATO**

I. **MAJUKUMU YA KAZI**

a) Kukusanya fedha kwa niaba ya Halmashauri kwa kuzingatia vyanzo vilivyoainishwa na sheria ndogo za Halmashauri.
b) Kuwasilisha fedha yote iliyokusanywa benki kila siku
c) Kuwasilisha ripoti ya makusanyo kwa watendaji wa kijiji au kwa Mkurugenzi Mtendaji au afisa yoyote aliyeidhinishwa
d) Kuwasilisha jina la mtu au kampuni iliyokaidi kulipa ushuru kwa makusudi
e) Kuwaelimisha walipa kodi juu ya umuhimu wa kulipa ushuru kwa hiari bila shuruti
f) Pamoja na klazi nyingine utakazopangiwa na mwajiri wako.

II. **SIFA ZA MUOMBAJI**

a) Muombaji awe ni Raia wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
b) Awe na elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea
c) Awe na uwezo wa kutumia simu janja (smartphone)
d) Awe na kitambulisho cha NIDA

1 Mtaa wa Utawala, 50118 Isinde, Mtapenda, S.L.P 688, Mpanda, Simu +255252955164, Nukushi +255252955164,
Barua pepe: ded@nsimbodc.go.tz, Tovuti: www.nsimbodc.go.tz

CamScanner

III. **MALIPO/POSHO**

Malipo/posho ni kiasi cha Shilingi laki mbili (200,000/=) za kitanzania kwa mwezi.

IV. **MASHARTI YA JUMLA**

a. Waombaji wote waambatishe barua za maombi na wasifu binafsi uliojitosheleza (Detail Curriculum Vitae) yenye anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na anuani ya Barua pepe (email address) pamoja majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika kama ni waajiriwa wa Serikali waambatanishe nakala za vitambulisho vya Kazi na kama sio mtumishi wa umma awe na mali isiyohamishika yenye thamani ya isiyopungua milioni 10

b. Maombi yote yaambatane na vyeti vya Elimu na Taaluma vilivyothibitishwa na mwanasheria /wakili ambavyo ni vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.

V. **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 16/02/2026**

VI. **MUHIMU;** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo,
S.L.P 688,
**MPANDA.**

VII. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hii **HAYATAFANYIWA KAZI.**

**Imetolewa na;**

Christina D. Bunini,
Mkurugenzi Mtendaji, MKURUGENZI MTENDAJI (W) NSIMBO
**NSIMBO**



CamScanner